


EPISCOPAL CHURCH of the
HEAVENLY REST

God's Love. For All.

2 Mbele ya Kuja
Ushirike Mtakatifu yaani Chakula cha Bwana
Jumapili, Novemba 19, 2023
Saa 1:00 Jioni



Second Sunday before Advent
The Holy Eucharist in Swahili
Sunday, Novemba 19, 2023
1:00 in the afternoon

WIMBO WA KUINGILIA

Wote kusimama

SHAIRI LA SIKU

Bwana ya majeshi amekusudia, na nani atamuzuiza? Na mukono wake umenyoshwa, na nani ataurudisha nyuma?

Isaya 14:28

MANENO YA KARIBU

Kasisi akaribishe watu na maneno haya:

Bwana awe nanyi.
Awe pia nawe.

SALA YA UNGAMO

Wote wapige magoti

Mungu Mwenyezi, kwa hivyo kwako mioyo yote ni wazi, mahitaji yote yamejulikana, wala hakuna siri lililofichwa; uyasafishe mawazo ya mioyo yetu kwa kuingiza Roho yako Mutakatifu, ili tukupende kwa ukamilifu na kulitukuza Jina lako takatifu, kama inavyotustahili; kwa Kristo Bwana wetu. Amina.

AMRI KUMI

Wote wapige magoti

Bwana wetu Yesu Kristo alisema, kama muginipenda mutatii mari zangu; afazali heri wale wenye kisikia Neno la Mungu na kulishika. Sikieni amri hizi Mungu alizoziagiza watu wake, na muziweke rohoni:

1. Mimi ni Bwana Mungu wako, usiwe na miungu mingine ila mimi. Upende Bwana Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili yako yote, na kwa nguvu yako yote.

Jibu Bwana, uturehemu, utuelekeze mioyo yetu tuishike amri hii.

2. Usijifanyie sanamu. Mungu ni roho, nao wenye kumwabudu, sharti wamwabudu katika roho na kweli.

Jibu Bwana, uturehemu, utuelekeze mioyo yetu tuishike amri hii.

3. Usilitaje jina la Bwana Mungu wako bule, lakini utolee Mungu kumwabudu kumupendeza, pamoja na heshima na woga.

Jibu Bwana, uturehemu, utuelekeze mioyo yetu tuishike amri hii.

4. Kumbuka siku ya Mungu uitakase. Kristo amefufuka, tia mafikili yako juu ya maneno ya juu, wala si juu ya maneno yaliyo duniani.

Jibu Bwana, uturehemu, utuelekeze mioyo yetu tuishike amri hii.

5. Heshimu baba yako na mama yako, uishi kama mutumishi wa Mungu, uheshimu watu wote, upende ndugu zako.

Jibu Bwana, uturehemu, utuelekeze mioyo yetu tuishike amri hii.

6. Usiue, jua lisishuke na uchungu wako haujakwisha bado, ushinde ubaya kwa mema.

Jibu Bwana, uturehemu, utuelekeze mioyo yetu tuishike amri hii.

7. Usizini, ujue mwili wako ni hekalu la Roho Mutakatifu aliye ndani yako.

Jibu Bwana, uturehemu, utuelekeze mioyo yetu tuishike amri hii.

PROCESSIONAL HYMN

Stand for the Procession

OPENING SENTENCE

The Lord of hosts has purposed, and who will hinder him? And his hand is stretched out, and who will turn it back?

Isaiah 14:28

OPENING ACCLAMATION

The Priest should welcome the people with these words::

The Lord be with you
And also with you.

THE COLLECT FOR PURITY

All kneel and say together

Almighty God, to you all hearts are open, all desires known, and from you no secrets are hid: Cleanse the thoughts of our hearts by the inspiration of your Holy Spirit, that we may perfectly love you, and worthily magnify your holy Name; through Christ our Lord. Amen.

THE DECALOGUE

Remain kneeling

Our Lord Jesus Christ said, if you love me you will obey my commandments; blessed are those who hear the Word of God and keep it. Hear these commands that God commanded his people, and keep them in your heart:

1. I am the Lord your God, you shall have none other gods but me. Love the Lord your God with all your heart, with all your soul, with all your mind, and with all your strength.

Answer **Lord have mercy upon us, and incline our hearts to keep this law.**

2. You shall not make to yourself any graven image. God is spirit, and those who worship him must worship in spirit and truth."

Answer **Lord have mercy upon us, and incline our hearts to keep this law.**

3. You shall not take the Name of the Lord your God in vain. Give pleasing worship to God with respect and fear.

Answer **Lord have mercy upon us, and incline our hearts to keep this law.**

4. Remember the Sabbath day and keep it holy. Christ is risen, set your thoughts on things above, not on things that are on earth.

Answer **Lord have mercy upon us, and incline our hearts to keep this law.**

5. Honor your father and your mother. Live as a servant of God, respect all people, and love your sisters and brothers.

Answer **Lord have mercy upon us, and incline our hearts to keep this law.**

6. You shall not commit murder. Do not let the sun go down on your anger. Overcome evil with good.

Answer **Lord have mercy upon us, and incline our hearts to keep this law.**

7. You shall not commit adultery. Know that your body is a temple of the Holy Spirit within you.

Answer **Lord have mercy upon us, and incline our hearts to keep this law.**

8. Usiibe, lakini zaidi utumike, ufanye kazi njema kwa mikono yako, uwe na kitu cha kugawia mwenye kuhitaji.

Jibu Bwana, uturehemu, utuelekeze mioyo yetu tuishike amri hii.

9. Usimushuhudie jirani yako uwongo, lakini useme kweli katika mapendo.

Jibu Bwana, uturehemu, utuelekeze mioyo yetu tuishike amri hii.

10. Usitamani chochote kilicho cha jirani yako. Kumbuka maneno ya Bwana Yesu, kama alivyosema: Upende jirani yako kama wewe mwenyewe, Basi, mapendo ni utimilifu wa sheria.

Jibu Bwana, uturehemu, tunakusihii uziandike amri zako hizi zote, mioyoni mwetu.

KUUNGAMA DHAMBI

Wote wapige magoti

Sikieni maneno ya Yohana Mtakatifu:

Kwa maana Mungu alivyopenda ulimwengu, hata kutoa Mwana wake wa pekee, ili kila mutu akimwamini asipotee, lakini apate uzima wa milele.

Yohana 3:16

Tunyamaze kidogo kukumbuka dhambi zetu

Wote wako kimya

Tukiri zambi zetu na kutubu na imani; tukikusudia kushika amri za Mungu na kukaa katika mapendo na salama na watu wote.

**Mungu Mwenyezi,
Baba yetu ya mbinguni,
tumekosea wewe,
na tumekosea jirani zetu
kwa mawazo yetu,
na kwa maneno yetu,
na kwa matendo yetu,
na kwa maovu tuliyoyatenda,
na kwa mema tusiyoyatenda,
kosa letu wenyewe.**

Sisi tunatubu kabisa.

**Kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo,
utusamehe yote yaliyopita;
utuwezeshe tangu leo kukutumikia,
katika upya wa uzima
kwa utukufu wa Jina lako. Amina.**

Mungu Mwenyezi, mwenye kusamehe wote wanaotubu kwa kweli; awarehemu, awasamehe, awaokoe kwa zambi zenu zote, awasibitisha, † awape nguvu kwa wema wote, na awalinde katika uzima wa milele; kwa Yesu Kristo Bwana wetu. **Amina.**

UTUKUFU

Wote kusimama

**Utukufu kwa Mungu, juu mbinguni,
na salama duniani,
kwa watu wanaomupendeza,**

8. You shall not steal. Rather, be useful, do good work with your hands, and have something to distribute to the needy.

Answer **Lord have mercy upon us, and incline our hearts to keep this law.**

9. You shall not bear false witness. Speak the truth in love.

Answer **Lord have mercy upon us, and incline our hearts to keep this law.**

10. You shall not covet anything that belongs to your neighbor. Remember the words of the Lord Jesus, as he said: Love your neighbor as yourself. Love, then, is the fulfillment of the law.

Answer **Lord have mercy upon us, and write all these your laws in our hearts, we ask you.**

CONFESSON OF SIN

Remain kneeling

Hear the words of Saint John:

God so loved the world that he gave his only Son, that whoever believes in him should not perish but have everlasting life.

John 3:16

Let us keep silence for a moment, to remember our sins.

All remain silent

Let us confess our sins, in penitence and faith, firmly resolved to keep God's commandments and to live in love and peace with all people.

**Almighty God,
our heavenly Father,
we have sinned against you,
and against our neighbors.
in our thoughts,
in our words,
in the evil that we have done,
and in the good that we have not done
through our own deliberate fault.
We truly repent of our sins.
For the sake of our Lord Jesus Christ,
forgive us all that is past;
enable us to serve you from now on,
in newness of life,
to the glory of your name. Amen.**

Almighty God, who forgives all who truly repent; have mercy upon you, pardon and deliver you from all your sins, confirm and strengthen you in all goodness, and keep you in eternal life; through Jesus Christ our Lord. **Amen.**

GLORY TO GOD

All Stand

**Glory to God in the highest,
and peace to his people on earth.
Lord God, heavenly King,**

tunakusifu, tunakubariki,
tunakuabudu, tunakutukuza,
tunakushukuru kwa ajili ya utukufu wako mkuu.
Bwana Mungu, Mufalme wa mbinguni,
Mungu Baba Mwenyezi,
Ee Bwana, Mwana pekee Yesu Kristo;
Ee Bwana Mungu, Mwana kondoo wa Mungu, Mwana wa Baba,
unayeondoa zambi za dunia, Uturehemu.
Unayeondoa zambi za dunia, upokee ombi letu.
Unayekaa kuume kwa Mungu Baba, Uturehemu.
Kwa maana wewe peke yako Mutakatifu,
wewe peke yako Bwana,
wewe peke yako, Ee Kristo,
pamoja na Roho Mutakatifu,
uliye juu kwa utukufu wa Mungu Baba. **Amina.**

KUPOKEA NENO LA MUNGU

Kasisi aseme SALA YA SIKU, akianza hivi:

Bwana awe nanyi.
Awe pia nawe.
Tuombe.

Mungu Mwenyezi, makusudi yako ya kifalme hayawezi kuzimika: utupatie imani kusimama imara kati ya masukosuko ya dunia hii, tukijua kwamba ufalme wako utakuja, na mapenzi yako yatatimzwa, kwa utukufu wako; kwa Yesu Kristo Bwana wetu, anayeishi na kutawala pamoja nawe na Roho Mutakatifu, Mungu mumoja sasa hata milele. **Amina.**

KWAYA AU WIMBO

SOMO LA KWANZA

Sefania 1:7,12-18

Kipande kinachotoka katika AGANO LA KALE kisomwe. Musomaji aseme kwanza:

Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa katika Kitabu cha Sefania.

Nyamaza kimya mbele za Bwana MUNGU; Kwa maana siku ya BWANA iko karibu; Kwa kuwa BWANA ametayarisha dhabihu, Amewatakasa wageni wake. Kisha itakuwa wakati ule, nitauchunguza Yerusalemu kwa taa; nami nitawaadhibu watu walioganda juu ya masira yao; wasemao katika mioyo yao, BWANA hatatenda mema, wala hatatenda mabaya. Na huko utajiri wao utakuwa mateka, na nyumba zao zitakuwa ukiwa; naam, watajenga nyumba, lakini hawatakaa ndani yake; nao watapanda mizabibu, lakini hawatakunywa divai yake. Hiyo siku ya BWANA iliyo kuu i karibu; I karibu, nayo inafanya haraka sana; Naam, sauti ya siku ya BWANA; Shujaa hulia kwa uchungu mwingi huko! Siku ile ni siku ya ghadhabu, Siku ya fadhaa na dhiki, Siku ya uharibifu na ukiwa, Siku ya giza na utusitusi, Siku ya mawingu na giza kuu, Siku ya tarumbeta na ya kamsa, Juu ya miji yenye maboma, Na juu ya minara mirefu. Nami nitawaletea wanadamu dhiki, hata watakwenda kama vipofu, kwa sababu wamemtenda BWANA dhambi; na damu yao itamwagwa kama mavumbi, na nyama yao kama mavi. Fedha yao wala dhahabu yao havitaweza kuwaokoa katika siku ile ya ghadhabu ya BWANA; bali nchi yote pia itateketezwa kwa moto wa wivu wake; maana atawakomesha watu wote wakao katika nchi hii, naam, mwisho wa kutisha.

almighty God and Father,
we worship you, we give you thanks,
we praise you for your glory.
Lord Jesus Christ, only Son of the Father,
Lord God, Lamb of God,
you take away the sin of the world:
have mercy on us;
you are seated at the right hand of the Father:
receive our prayer.
For you alone are the Holy One,
you alone are the Lord,
you alone are the Most High, Jesus Christ,
with the Holy Spirit,
in the glory of God the Father. Amen.

THE LITURGY OF THE WORD

The Priest says the Collect of the Day, beginning with this:

The Lord be with you.

And also with you.

Let us pray.

Almighty God, your royal purposes cannot be extinguished: give us faith to stand firm in the midst of the turmoil of this world, knowing that your kingdom will come, and your will will be fulfilled, for your glory; through Jesus Christ our Lord, who lives and reigns with you and the Holy Spirit, one God now and forever. **Amen.**

CHOIR OR HYMN

THE FIRST READING

Zephaniah 1:7, 12-18

All sit. A passage from the Old Testament is read. The reader first says:

Hear the word of the Lord as it is written in the Book of Zephaniah.

Be silent before the Lord God! For the day of the Lord is at hand; the Lord has prepared a sacrifice, he has consecrated his guests. At that time I will search Jerusalem with lamps, and I will punish the people who rest complacently on their dregs, those who say in their hearts, "The Lord will not do good, nor will he do harm." Their wealth shall be plundered, and their houses laid waste. Though they build houses, they shall not inhabit them; though they plant vineyards, they shall not drink wine from them. The great day of the Lord is near, near and hastening fast; the sound of the day of the Lord is bitter, the warrior cries aloud there. That day will be a day of wrath, a day of distress and anguish, a day of ruin and devastation, a day of darkness and gloom, a day of clouds and thick darkness, a day of trumpet blast and battle cry against the fortified cities and against the lofty battlements. I will bring such distress upon people that they shall walk like the blind; because they have sinned against the Lord, their blood shall be poured out like dust, and their flesh like dung. Neither their silver nor their gold will be able to save them on the day of the Lord's wrath; in the fire of his passion the whole earth shall be consumed; for a full, a terrible end he will make of all the inhabitants of the earth.

Na kwa mwisho aseme:

Hilo ndilo Neno la Bwana.

Asante kwa Mungu.

WIMBO

SOMO LA PILI

Wathesalonike 5:1-11

Kipande kinachotoka katika AGANO JIPIYA kisomwe. Musomaji aseme kwanza:

Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa katika Barua ya Paulo Mtume kwa Wafilipi.

Lakini, ndugu, kuhusu nyakati na majira, hamna haja niwaandikie. Maana ninyi wenyewe mna-jua hakika ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwizi ajavyo usiku. Wakati wasemapo, Kuna amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafla, kama vile uchungu umjiavyo mwenye mimba, wala hakika hawataokolewa. Bali ninyi, ndugu, hamko gizani, hata siku ile iwapate kama mwizi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi si wa usiku, wala wa giza. Basi tusilale usingizi kama wengine, bali tukeshe, na kuwa na kiasi. Maana walalao usin-gizi hulala usiku, pia na walewao hulewa usiku. Lakini sisi tulio wa mchana, tuwe na kiasi, hali tukijivika kifuani imani na upendo, na chapeo yetu iwe tumaini la wokovu. Kwa kuwa Mungu hakutuweka ili tupate hasira yake, bali ili tupate wokovu, kwa Bwana wetu Yesu Kristo; ambaye alikufa kwa ajili yetu, ili tuishi pamoja naye, iwe tunakesha au tunalala. Basi, farijianeni na ku-jengana kila mtu na mwenzake, hakika kama mnavyofanya.

Na kwa mwisho aseme:

Hilo ndilo Neno la Bwana.

Asante kwa Mungu.

WIMBO

HABARI NJEMA

Mathayo 25:14-30

Kipande cha HABARI NJEMA kisomwe. Musomaji aseme kwanza:

Sikieni Habari Njema takatifu kama lilivyoandikwa katika Injili ya Matayo Mtakatifu.

Utukufu uwe nawe, Ee Bwana wetu.

Maana itakuwa kama mfano wa mtu aliyetaka kusafiri, akawaita watumwa wake, akaweka kwao mali zake. Akampa mmoja talanta tano, na mmoja talanta mbili, na mmoja talanta moja; kila mtu kwa kadiri ya uwezo wake; akasafiri. Mara yule aliyepokea talanta tano akaenda, akafanya biashara nazo, akachuma faida talanta nyingine tano. Vile vile na yule mwenye mbili, yeye naye akachuma nyingine mbili faida. Lakini yule aliyepokea moja alikwenda akafukua chini, akaificha fedha ya bwana wake. Baada ya siku nyingi akaja bwana wa watumwa wale, akafanya hesabu nao. Akaja yule aliyepokea talanta tano, akaleta talanta nyingine tano, akisema, Bwana, uliweka kwangu talanta tano; tazama, talanta nyingine tano nilizopata faida. Bwana wake akamwambia, Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako. Akaja na yule aliyepokea talanta mbili, akasema, Bwana, uliweka kwangu talanta mbili; tazama, talanta nyingine mbili nilizopata faida. Bwana wake akamwambia, Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako. Akaja na yule aliyepokea talanta moja, akasema, Bwana, nilitambua ya kuwa wewe u mtu mgumu, wavuna usipopanda, wakusanya usipotawanya; basi nikaogopa, nikaenda nikaificha talanta yako katika ardhi; tazama, unayo iliyo yako. Bwana

At the end the reader says:

This is the Word of the Lord.

Thanks be to God.

HYMN

SECOND READING

I Thessalonians 5:1-11

All Sit. A passage from the New Testament is read. The reader first says:

Hear the word of the Lord as it is written in the Letter of the Apostle Paul to the Philippians.

Now concerning the times and the seasons, brothers and sisters, you do not need to have anything written to you. For you yourselves know very well that the day of the Lord will come like a thief in the night. When they say, "There is peace and security," then sudden destruction will come upon them, as labor pains come upon a pregnant woman, and there will be no escape! But you, beloved, are not in darkness, for that day to surprise you like a thief; for you are all children of light and children of the day; we are not of the night or of darkness. So then let us not fall asleep as others do, but let us keep awake and be sober; for those who sleep sleep at night, and those who are drunk get drunk at night. But since we belong to the day, let us be sober, and put on the breastplate of faith and love, and for a helmet the hope of salvation. For God has destined us not for wrath but for obtaining salvation through our Lord Jesus Christ, who died for us, so that whether we are awake or asleep we may live with him. Therefore encourage one another and build up each other, as indeed you are doing.

At the end the reader says:

This is the Word of the Lord.

Thanks be to God.

HYMN

THE GOSPEL READING

Matthew 25:14-30

All Stand. A passage from a Gospel is read. The reader first says:

Hear the holy Gospel, as it is written in the Gospel of St. Matthew.

Glory be to you, O Lord.

Jesus said, "It is as if a man, going on a journey, summoned his slaves and entrusted his property to them; to one he gave five talents, to another two, to another one, to each according to his ability. Then he went away. The one who had received the five talents went off at once and traded with them, and made five more talents. In the same way, the one who had the two talents made two more talents. But the one who had received the one talent went off and dug a hole in the ground and hid his master's money. After a long time the master of those slaves came and settled accounts with them. Then the one who had received the five talents came forward, bringing five more talents, saying, 'Master, you handed over to me five talents; see, I have made five more talents.' His master said to him, 'Well done, good and trustworthy slave; you have been trustworthy in a few things, I will put you in charge of many things; enter into the joy of your master.' And the one with the two talents also came forward, saying, 'Master, you handed over to me two talents; see, I have made two more talents.' His master said to him, 'Well done, good and trustworthy slave; you have been trustworthy in a few things, I will put you in charge of many things; enter into the joy of your master.' Then the one who had received the one talent also came forward, saying, 'Master, I knew that you were a harsh man, reaping where you did not sow, and gathering where you did not scatter seed; so I was afraid, and I went and hid your talent

wake akajibu, akamwambia, Wewe mtumwa mbaya na mlegevu, ulijua ya kuwa navuna nisipopanda, nakusanya nisipotawanya; basi, ilikupasa kuiweka fedha yangu kwa watoao riba; nami nikija ningalipata iliyo yangu na faida yake. Basi, mnyang'anyeni talanta hiyo, mpeni yule aliye nazo talanta kumi. Kwa maana kila mwenye kitu atapewa, na kuongezewa tele; lakini asiye na kitu, hata kile alichochacho atanyang'anywa. Na mtumwa yule asiye faa, mtupeni mbali katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.

Mwisho wa kusoma Habari Njema, musomaji aseme:

Hii ndiyo Habari Njema ya Kristo.

Tunakusifu sana, Ee Kristo, kwa Habari Njema yako takatifu.

WIMBO WA INJILI

KUHUBIRI

Mchungaji David Romanik

IMANI YA NIKE

Wote kusimama

Ninamwamini Mungu mumoja, Baba Mwenyezi,
Muumba wa mbingu na dunia,
na vitu vyote vinavyoonekana na visivyoonekana.

Ninamwamini Bwana mumoja, Yesu Kristo,
Mwana wa pekee wa Mungu,
amezaliwa na Baba mbele ya kuwa ulimwengu,
Mungu kutoka Mungu, Nuru kwa Nuru,
Mungu kweli kwa Mungu kweli,
amezaliwa, hakuumbwa,
Mwenye umungu mumoja na Baba.
Vitu vyote viliumbwa naye.
Alishuka toka mbinguni,
kwa ajili ya sisi watu, na kwa ajili ya wokovu wetu;
alitwaa mwili kwa tendo la Roho Mutakatifu,
katika Bikira Maria, akawa mutu.
Akasulibiwa kwa ajili yetu, wakati wa Pontio Pilato,
akateswa, akazikwa, Akafufuka kisha siku tatu, kama ilivyoandikwa;
akapanda mbinguni, anakaa kwa mukono wa kuume kwa Baba.
Ndipo atarudi kwa utukufu,
kuwahukumu wazima na wafu,
na ufalme wake hautakuwa na mwisho.

Ninamwamini Roho Mutakatifu,
Bwana na Mutoa uzima,
aliyetoka kwa Baba na Mwana,
anayeabudiwa na kutukuzwa,
pamoja na Baba na Mwana,
aliyesema kwa manabii.

in the ground. Here you have what is yours.’ But his master replied, ‘You wicked and lazy slave! You knew, did you, that I reap where I did not sow, and gather where I did not scatter? Then you ought to have invested my money with the bankers, and on my return I would have received what was my own with interest. So take the talent from him, and give it to the one with the ten talents. For to all those who have, more will be given, and they will have an abundance; but from those who have nothing, even what they have will be taken away. As for this worthless slave, throw him into the outer darkness, where there will be weeping and gnashing of teeth.’”

After reading the Gospel, the reader says:

This is the Gospel of Christ.

Praise be to you, O Christ, for your holy Gospel.

A HYMN OF THE GOSPEL

SERMON

The Rev'd David Romanik

THE NICENE CREED

All Stand

We believe in one God,
the Father, the Almighty,
maker of heaven and earth,
of all that is, seen and unseen.

We believe in one Lord, Jesus Christ,
the only Son of God,
eternally begotten of the Father,
God from God, Light from Light,
true God from true God,
begotten, not made,
of one Being with the Father.
Through him all things were made.
For us and for our salvation
he came down from heaven:
by the power of the Holy Spirit
he became incarnate from the Virgin Mary,
and was made man.
For our sake he was crucified under Pontius Pilate;
he suffered death and was buried.
On the third day he rose again
in accordance with the Scriptures;
he ascended into heaven
and is seated at the right hand of the Father.
He will come again in glory to judge the living and the dead,
and his kingdom will have no end.

We believe in the Holy Spirit, the Lord, the giver of life,
who proceeds from the Father and the Son.
With the Father and the Son he is worshiped and glorified.

Ninaamini Kanisa, moja, takatifu, katolika,‡
lililotoka kwa Mitume.
Ninasadikia ubatizo mumoja
kwa kuondolewa kwa zambi.
Ninangojea ufufuko wa wafu
na uzima wa milele utakaokuja. **Amina.**

MAOMBI YA KANISA

Wote wapige magoti

Tuombe Kanisa na dunia na tumushukuru Mungu kwa wema wake wote.

Tukumbuke waaskofu wote, na hasa Askofu Mukuu yetu Michael, na Askofu ya Dayosisi yetu Scott, na waongozi wengine wa makanisa yote: wawe na hekima na umoja.

Bwana mwema utusikie.

Wakubwa wa inchi yetu watawale na haki.

Bwana mwema utusikie.

Haki iwe ngabo na mulinzi wetu.

Bwana mwema utusikie.

Inchi iwe salama; na watu wabarikiwe.

Bwana mwema utusikie.

Makundi ya wanyama yaongezeke; na samaki baharini ziwe nyingi.

Bwana mwema utusikie.

Mashamba yazae matunda tele; mavuno yawe mengi.

Bwana mwema utusikie.

Mafundi na wafanya biashara wote waone faida kwa kazi zao.

Bwana mwema utusikie.

Sisi na adui zetu tuwe na moyo wa kuvunjika na tutafute salama.

Bwana mwema utusikie.

Nguvu ya Bwana itegemeze wagonjwa wote.

Bwana mwema utusikie.

Mapendo ya Bwana yafariji waliokufliwa, wanaoteswa, wajane, yatima, na wenye kusikia upekee.

Bwana mwema utusikie.

Njia za dunia zisafishwe kwa hatari zo zote.

Aleluya. Bwana wa rehema ni pamoja nasi. Amina.

Muhudumu anaweza kualika watu wengine kuomba na maneno haya:

Tuendeleo kuomba, kwa sisi wenyewe na ndugu na dada zetu...

Mu Kuchunga kimya: wengine wanaweza kuomba kwa sauti, moja kwa moja, wengine kwa siri.

Nyuma ya dakika chache muhudumu asemi:

Tumaini letu ni kwako, Bwana wa rehema.

Tunategemea wewe pekee, Bwana wa mapendo. Amina.

He has spoken through the Prophets.
We believe in one holy catholic and apostolic Church.
We acknowledge one baptism for the forgiveness of sins.
We look for the resurrection of the dead,
and the life of the world to come. Amen.

THE PRAYERS OF THE CHURCH

All Kneel

Let us pray for the Church and for the world, and let us thank God for his goodness.

We remember all bishops, especially our Presiding Bishop Michael, and the Bishop of our Diocese Scott, and the leaders of all the churches: may they be blessed with wisdom and unity.

Good Lord, hear us.

May the leaders of our country rule with justice.

Good Lord, hear us.

May righteousness be our shield and our protector.

Good Lord, hear us.

May the country be at peace; and the people be blessed.

Good Lord, hear us.

May the herds increase; and the fish in the lakes be many.

Good Lord, hear us.

May the fields yield abundantly; may the harvests be great.

Good Lord, hear us.

May all artisans and traders see the benefit of their labors.

Good Lord, hear us.

May we and our enemies turn from strife and seek peace.

Good Lord, hear us.

May the strength of the Lord support all who are sick.

Good Lord, hear us.

May the Lord's love comfort the bereaved, the oppressed, widows, orphans, and the lonely.

Good Lord, hear us.

May the paths and roads of the world be swept clean of all dangers.

Alleluia. The Lord of mercy is with us. Amen.

The minister may invite others to pray, using these words:

Let us continue to pray for ourselves and for our brothers and sisters...

In a time of quiet, some may pray out loud, one at a time, and others may pray in secret.

After a few minutes, the minister may say:

Our trust is in you, merciful Lord

We rely on you alone, O God of love. Amen.

SALA YA BWANA

Mhudumu aseme:

Tuombe, kama Mwokozi wetu alivyotuagiza na namna alivyotufundisha, tusubutu kusema:

Wote:

Baba yetu, uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, duniani kama mbinguni. Utupe leo chakula chetu cha kila siku; utusamehe makosa yetu, kama tunavyowasamehe waliotukosea. Usitulete katika majaribu, lakini utuokoe katika uovu. Kwani kwako ufalme, uwezo na utukufu, milele na milele, Amina.

SALAMA YA BWANA

Wote wasimame. Mbele ya kuwatakia salama, Kasisi aseme moja kati ya matangulizi haya (kufuatana na wakati wa mwaka au neno kubwa la mahubiri):

Kristo ni salama yetu. Ametupatanisha na Mungu katika mwili mumoja, kwa njia ya musalaba wake. Tunakutana katika jina lake, tukifurahi pamoja katika salama yake.

Waefeso 2:16

Salama ya Bwana iwe nanyi siku zote.

Iwe pia nawe.

Kasisi anaweza kusema:

Katika mapendo ya Kristo, tupeane salama.

Watu wasalamiane.

BARAKA YA WATOTO

Watoto wote wanaalikwa kufika mbele ya kanisa ili wabarikiwe na kasisi.

SHEREHE YA MEZA YA BWANA

Kasisi atayarisha mukate na mvinyo kwa Meza Takatifu, watu wakiimba wimbo, na kutoa sadaka. Kasisi aombe sadaka.

Wote kusimama.

Kasisi Bwana awe nanyi

Wote **Awe pia nawe.**

Kasisi Inueni mioyo yenu.

Wote **Tunaiinua kwa Bwana.**

Kasisi Tumushukuru Bwana Mungu wetu.

Wote **Kutenda hivi ni vizuri na vema.**

Kasisi:

Ndiyo bora kwetu, inatupasa, ni furaha yetu, kila wakati na ndani ya kila pahali, kukushukuru Ee Bwana, Baba Mutakatifu, Mungu Mwenyezi wa milele, kwa Yesu Kristo, Mwana wako wa pekee, Bwana wetu.

Kwani yeye ni Neno lako la uzima, kwa yeye vitu vyote viliumbwa toka mwanzo, nasi tumeumbwa kwa mufano wako. Kwa yeye ulituokoa toka utumwa wa zambi; ukimupa kuzaliwa mutu, kufa musalabani na kufufuka kwa sisi.

Kwa yeye umetufanya kuwa watu wako pekee, ukimutukuza juu kwa mukono wako wa kuume wa utukufu; na kwa yeye umetutumia sisi Roho yako Mutakatifu ya uzima.

Kushukuru kwa nyakati fulani:

Kwa hivyo sisi pamoja na malaika na malaika wakuu, na kundi lote la mbinguni, tunakutukuza na kulisifu jina lako takatifu. Tunakusifu daima, tukisema:

THE LORD'S PRAYER

The minister says:

As our Savior commanded and taught us, we are bold to say:

All say:

Our Father in heaven, hallowed be your name, your kingdom come, your will be done, on earth as in heaven. Give us today our daily bread. Forgive us our sins as we forgive those who sin against us. Lead us not into temptation but deliver us from evil. For the kingdom, the power, and the glory are yours now and forever. Amen.

THE PEACE OF THE LORD

All stand. Before greeting the people, the Priest says one of these introductions (chosen according to the season or theme of the service):

Christ is our peace. He has reconciled us to God in one body by his cross. We meet in his name and rejoice together in his peace

based on Ephesians 2:16

The peace of the Lord be always with you.

And also with you.

The Priest may say:

In the love of Christ, let us give one another peace.

The people greet each other.

BLESSING OF THE CHILDREN

All children are invited to come to the front of the church to be blessed by the priest.

THE LITURGY OF THE EUCHARIST

The priest prepares the bread and wine on the Holy Table, while the people sing a hymn, and give their offerings. The priest prays over the offerings.

All Stand

Priest The Lord be with you.

All **And with your spirit.**

Priest Lift up your hearts.

All **We lift them to the Lord.**

Priest Let us give thanks to the Lord our God.

All **It is good and right so to do.**

The priest says:

Indeed, it is best for us, it is our duty and our joy, at all times and in all places, to thank you O Lord, Holy Father, almighty and eternal God, through Jesus Christ, your only Son our Lord.

For he is you living Word, through him you have created all things from the beginning, and formed us in your own image. Through him you have saved us from the slavery of sin, giving him a human birth, to die upon the cross, and to rise again for us.

Through him you have made us your own people, exalting him to your right hand on high; and through him you have sent us your Holy Spirit of life.

Here a Proper Preface is said:

Therefore with angels and archangels, and with all the company of heaven, we exalt and praise your holy name. We praise you forever, saying:

Wote:

**Mutakatifu, Mutakatifu, Mutakatifu,
Bwana Mungu wa uwezo na mamlaka,
mbingu na inchi zimejaa utukufu wako,
utukufu uwe nawe, Ee Bwana uliye mbinguni.
Abarikiwe anayekuja kwa Jina la Bwana.
Hosana juu mbinguni.**

Wote wapige magoti

Ee Baba ya mbinguni, upokee kusifu kwetu katika Mwana wako, Mwokozi wetu Yesu Kristo, na tukipokea mukate huu na kikombe hiki kama Mwana wako alivyotuamuru, tuwe washiriki wa mwili na damu yake.

Usiku ule alipotolewa alitwaa mukate na alipokwisha kukushukuru, akauvunja akawapa wanafunzi wake akisema: «Twaeni, mule, huu ni Mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi.»

Ndivyo, walipokwisha kula, akatwaa kikombe; alipokwisha kukushukuru, akawapa, akisema: «Ninyi wote munywe hii, kwani hii ndiyo Damu yangu ya Agano Jipya, inayomwangika kwa ajili yenu, na kwa watu wengi, kwa kusamehewa kwa zambi; fanyeni hivi, kila mara munapoikunywa kwa kunikumbuka mimi.»

Wote:

**Kristo alikufa;
Kristo amefufuka;
Kristo atakuja tena.**

Kasisi:

Ndiyo Baba ya mbinguni, kwa mukate huu na kikombe hiki tunafanya hivi kumukumbuka. Tunaonyesha na kutangaza zabihu yake kamilifu musalabani mara moja; tunatangaza ufufuko wake toka wafu, na kupanda kwake mbinguni, na tunangojea kuja kwake katika utukufu.

Katika yeye, kuhani yetu mukubwa, upokee zabihu yetu ya kusifu na kushukuru, na kwa kula na kunywa zawadi hizi takatifu, mbele ya utukufu wako, tuwe wapya kwa Roho yako; utuingize mapendo yako, na utuunge pamoja katika mwili wa Mwana wako.

Naye, na katika yeye, na kwa uwezo wa Roho Mutakatifu, pamoja na wote wenye kusimama mbele yako, kwa inchi na mbingu, tunakuabudu, Baba Mwenyezi, sasa hata milele:

Wote:

Baraka na heshima, na utukufu na uwezo, uwe kwako milele na milele. Amina.

Kasisi:

Tujitayarishe kupokea Chakula cha Bwana:

Wote:

Hatusubutu kuikaribia Meza yako hii, Bwana mwenye rehema, kwa kuitumainia haki yetu wenyewe, ila rehema zako nyingi zilizo kubwa. Hatustahili hata kuokota makombo chini ya Meza yako. Ndiwe Bwana usiyegeuka, asili yako ni kuwa na rehema daima. Basi utupe, Bwana mwema, tuule mwili wa Mwana wako mupendwa Yesu Kristo, na kuinywa damu yake, tukae daima ndani yake, naye ndani yetu. Amina.

Kasisi:

Mukaribie na imani, mupokee sakramento hii takatifu ya mwili na damu ya Kristo tukikumbuka alikufa kwa ajili yetu na tumule mioyoni mwetu kwa imani tukishukuru.

Halafu wahudumu wagawe mukate na mvinyo kwa watu. Wakati watu wanapokea, kwanza iwe kimya, lakini nyuma kidogo nyimbo za hali ya maombi zinaweza kuimbwa.

All say:

**Holy, Holy, Holy,
Lord God of power and might,
heaven and earth are full of your glory.
Glory be to you, O Lord in heaven.
Blessed is he who comes in the name of the Lord.
Hosanna in the highest.**

All Kneel

Accept our praises, O heavenly Father, through your Son, our Savior Jesus Christ, and as we receive this bread and this cup as your Son commanded us, may we be partakers of his body and his blood.

On the same night that he was betrayed, he took bread and after giving you thanks he broke it and gave it to his disciples saying, "Take, eat, this is my Body which is given for you; do this in remembrance of me."

In the same way, when they had eaten, he took the cup; and after giving you thanks, he gave it to them saying, "Drink this all of you, for this is my Blood of the New Covenant, which is shed for you, and for many, for the forgiveness of sins; do this, as often as you drink it, in remembrance of me."

All say:

**Christ has died;
Christ is risen;
Christ will come again.**

The Priest continues:

Indeed, heavenly Father, with this bread and this cup we do this in remembrance of him. We show and proclaim his perfect sacrifice made once for all on the cross; we proclaim his resurrection from the dead, and his ascension into heaven; and we wait for his coming in glory.

Accept through him, our high priest, this our sacrifice of praise and thanks, and as we eat and drink these holy gifts, in the presence of your majesty, renew us by your Spirit, inspire us with your love, and unite us in the body of your Son.

With him and through him, by the power of the Holy Spirit, with all who stand before you in earth and heaven, we worship you, Father Almighty, now and forever:

All say:

Blessing and honor, and glory and power, be yours forever and ever. Amen.

The Priest says:

Let us prepare to receive the Lord's meal:

All say:

We do not presume to come to this your table, merciful Lord, trusting in our own righteousness, but in your manifold and great mercies. We are not worthy so much as to gather up the crumbs under your table. But you are the same Lord whose nature is always to have mercy. Grant us therefore, gracious Lord, so to eat the flesh of your dear Son Jesus Christ and to drink his blood, that we may evermore dwell in him and he in us. Amen.

The Priest says:

Draw near with faith, receive this holy sacrament of the body and blood of Christ as we remember that he died for our sake, and feed on him in our hearts by faith with thanksgiving.

Then the ministers distribute the bread and wine to the people. While the people are receiving, silence should be kept at first, but later prayerful songs may be sung.

KUTOKA KWA WATU WA MUNGU

Wote wapige magoti. Wote waseme moja la maombi haya:

**Mungu Mwenyezi,
tunakushukuru kwa kutulisha
na mwili na damu ya Mwana wako, Yesu Kristo.
Kwa yeye tunakutolea mioyo na miili yetu
kuwa zabihu iliyo hai.
Ututume duniani
kwa uwezo wa Roho yako,
kuishi na kutumika,
kwa sifa na utukufu wako. **Amina.****

SHAIRI LA SIKU

Shairi la kila wakati lisomwe.

Ninyi wote ni wana wa nuru, na wana wa muchana: basi tusilale usingizi, lakini tuagalie na kuwa na kiasi.

2 Watesalonika 5:5,6

SALAMA NA BARAKA

Wote wapige magoti. Kasisi au Askofu akiwapo, aseme Salama na Baraka, au Baraka ya kila wakati.

Salama ya Mungu, inayopita akili yote, iwalinde mioyo na nia zenu, katika hali ya kujua na kupenda Mungu, na Mwana wake, Yesu Kristo Bwana wetu; na baraka ya Mungu Mwenyezi, Baba na Mwana, na Roho Mutakatifu, iwe kwenu na ikae nanyi, milele na milele. **Amina.**

Wote kusimama.

Muhudumu aondoe watu na maneno haya:

MANENO YA KUAGANA

Bwana wetu akae nanyi.

Akae na roho yako.

Kwendeni na salama kwa kumupenda na kumutumikia Bwana.

Kwa Jina la Kristo. Amina.

Wimbo wa kumaliza ibada.

WIMBO YA KUTOKA

THE GOING OUT OF THE PEOPLE OF GOD

All kneel. All say this prayer:

**Almighty God,
we thank you for feeding us
with the body and blood of your Son, Jesus Christ.
Through him we offer you our souls and bodies
to be a living sacrifice.
Send us out into the world
in the power of your Spirit,
to live and work to your praise and glory. Amen.**

CLOSING SENTENCE

An appropriate sentence may be said.

You are all children of light, and children of the day: so let us not sleep, but watch and be sober.
2 Thessalonians 5:5,6

THE BLESSING

All kneel. The Priest, or the Bishop if present, says the Peace and Blessing, or a seasonal blessing.

The peace of God, which passes all understanding, keep your hearts and minds in the knowledge and love of God, and of his Son Jesus Christ our Lord; and the blessing of God almighty, the Father, the Son, and the Holy Spirit, be among you, and remain with you always. **Amen.**

All Stand.

A minister dismisses the people with these words:

WORDS OF DISMISSAL

The Lord be with you.

And with your spirit.

Go in peace to love and serve the Lord.

In the name of Christ. Amen.

A song is sung to end the service.

RECESSIONAL HYMN

WAHUDUMU WA LITURUJIA

Waziri/Minister - Pastor Bikole Mulanda, Swahili Minister

Muhubiri na Muhudumu/Celebrant & Preacher - The Rev'd David Romanik, Rector

Kwaga/Music - Alleluia Choir

Wasindikizi na Wasomaji/Lay Ministers - Bijoux Estella, Batumike Fatuma Ruth

Teknologia/Sound - Bill Young

Washemasi/Greeters & Ushers - Baya Lushiawe



602 Meander Street Phone: (325) 677-2091
Abilene, Texas 79602 Email: info@heavenlyrestabilene.org
Website: heavenlyrestabilene.org Social media: [@heavenlyrestabilene](https://www.instagram.com/heavenlyrestabilene)

CLERGY AND STAFF

The Reverend David F. Romanik, <i>Rector</i>	Carol Ann Weston, <i>Director of Family Ministries</i>
The Reverend Corrie Cabes, <i>Associate Rector</i>	Luke Mendez, <i>Coordinator for Youth and Children's Ministry</i>
The Reverend Amanda Watson, <i>Assistant Rector for Community Life</i>	Steve Gibbs, <i>Parish Coordinator</i>
The Reverend Dr. Doug Thomas, <i>Priest in Residence</i>	LeighAnna Morris, <i>Parish Accountant</i>
The Reverend Karen Boyd, <i>Deacon</i>	Austin Hackel, <i>Communications Coordinator</i>
The Reverend Dr. Russell Dickerson, <i>Deacon</i>	Robert Becerra, <i>Sexton</i>
Bikole Mulanda, <i>Swahili Minister</i>	Adrian Smith, <i>Assistant Sexton</i>
Thomas Pavlechko, <i>Organist and Director of Music</i>	Dorothy Guerra, <i>Housekeeper</i>
Shelly Reed, <i>Children's Music Assistant</i>	Anne Jones, <i>Nursery Manager</i>

VESTRY AND APPOINTED OFFICERS

Annabel House, *Senior Warden*; Harry Hurt, *Junior Warden*; Debbie Sherman, *Secretary*; Connie Collier, Sarah Ferguson, Lisa Goolsby, Kate Haney, Jay Hardaway, Norene Mansell, John Nichols, Robert Peterson, Darryl Tippens, Elizabeth Niblo Wallace, *Chancellor*; and Sam Cutbirth, *Treasurer*